

Maelezo ya Ukweli Kuhusu COVID-19 Chanjo ya COVID-19 ya Johnson & Johnson Imesitishwa Ohio

Mnamo Aprili 13, 2021, Gavana Mike DeWine, Mkurugenzi wa Idara ya Afya ya Ohio Stephanie McCloud, na Afisa Mkuu wa Matibabu wa Idara ya Afya ya Ohio Bruce Vanderhoff, M.D., aliwashauri watoaji wote wa chanjo ya COVID-19 wa jimbo la Ohio waache kutumia chanjo ya Johnson & Johnson (Janssen) kwa muda.

Hii inatokana na pendekezo la Mamlaka ya Marekani ya Chakula na Dawa (FDA) na Vituo vya Kudhibiti na Kuzuia Magonjwa (CDC) [la kusitisha kutumia chanjo ya Johnson & Johnson](#) ili ichunguzwe zaidi baada ya watu sita nchini Marekani kuganda damu ambayo si kawaida baada ya kupokea chanjo.

Kuganda damu ambayo si kawaida iliripoti kwamba

Takriban dozi milioni 6.8 za chanjo ya Johnson & Johnson ya COVID-19 zimeshatolewa nchini Marekani mpaka sasa. Wagonjwa sita ambao damu yao iliganda kwa hali ya mvilio kwenye mishipa ya damu ubongoni (CVST) walionekana kuwa pia na viwango vya chini vya chembe za damu (thrombocytopenia), kulingana na FDA na CDC. Hali hii si ya kawaida. Wagonjwa hawa wote sita walikuwa wanawake wenye umri wa miaka kati ya 18-48. Dalili zilitokea baada ya siku sita mpaka 13 baada ya chanjo, na mtu mmoja alifariki.

Kulingana na CDC, matibabu yanayopendekezwa kwa aina hii mahususi ya kuganda kwa damu ni tofauti na matibabu ya kawaida yanayoweza kutolewa ya kuganda kwa damu. Kwa kawaida, dawa ya kuzuia damu kuganda inayoitwa heparin hutumiwa kutibu kuganda kwa damu. Katika hali hii, kutoa dawa ya heparin kunaweza kuwa hatari, na matibabu mbadala yanahitaji kut.

Chanjo ya Johnson & Johnson hutumia aina ya virusi iliyobadilishwa kuagiza seli zitengeneza nakala za protini ya spike kwenye SARS-CoV-2 (virusi inayosababisha COVID-19).

Virusi amilifu, kama vile vinavyosababisha mafua, hutumiwa kama wadudu wanaosambaza ugonjwa (au kifaa cha usafirishaji) ili kutoa maelekezo ya kutengeneza protini ya spike.

Mwili unaona protini kama mvamizi na kuundaa kinga ya kupigana naye.

Hatua zinazofuata

Kamati ya Ushauri ya CDC kuhusu Shughuli za Chanjo (ACIP) ilikutana mnamo Jumatano, Aprili 14, kwa ajili ya kukagua wagonjwa hao na kuchunguza umuhimu wake unaoweza kutokea. Kamati haikutoa mapendekezo yoyote kwa CDC, na imepanga kukutana tena takriban siku 7-10 baada ya uchambuzi kamili wa faida na hatari kukamilika. FDA itakagua uchambuzi huo kwa kuwa inachunguza pia wagonjwa hawa. Utaoji wa chanjo ya Johnson & Johnson bado unaendelea kusitishwa kwa muda.

Je, hili linamaanisha nini kwa watu ambao wamepokea chanjo ya Johnson & Johnson?

Kulingana na CDC, hatari ya kupata hali hizi ni ndogo sana kwa watu waliopata chanjo hiyo zaidi ya mwezi mmoja uliopita. Ikiwa ulipokea chanjo ya Johnson & Johnson hivi karibuni **indani ya wiki tatu zilizopita**, CDC inapendekeza upate matibabu ukiwa na maumivu makali ya kichwa, maumivu ya tumbo, maumivu mguuni, au ukishindwa kupumua .

Watu hawapaswi kuwa na wasiwasi kuhusu maumivu madogo ya kichwa au dalili kama za mafua katika siku chache baada ya chanjo. Dalili hizo ni za kawaida, ni dalili zisizo na madhara zinazosababishwa na jinsi ambavyo mfumo wa kinga unapambana na chanjo.

Je, watu wanapaswa kufanya nini ikiwa wamepangiwa kupokea chanjo ya Johnson & Johnson?

Wagonjwa wanaotarajia kwenda kwenye miadi ya kupokea chanjo ya Johnson & Johnson wanapaswa kuwasiliana na mtoaji wao kwa ajili ya mwongozo wa haraka kuhusu kupanga tena. Ikiwa watoaji huduma hawawezi kufikia chanjo ya dozi mbili ya Moderna au Pfizer kwa haraka, huenda wagonjwa watafuta miadi yao au itapangwa tena katika tarehe ya baadaye.

Chanjo za Moderna na Pfizer zinatumia teknolojia tofauti na chanjo ya Johnson & Johnson. Hakujuwa na mashaka ya usalama katika majaribio ya kliniki au tangu idhini ya matumizi ya dharura ya chanjo za messenger RNA (mRNA). Chanjo za MRNA hutumia nyuzi za jenetiki kutoa msimbo wa jenetiki kwenye seli ili kutengeneza protini ya spike katika virusi vya SARS-CoV-2. Protini zilizotengenezwa kwa maelekezo ya mRNA huuwasha mfumo wa kinga, kuufunza kutambua protini ya utando kama adui, na kubuni kingamwili za kupambana nayo.

Uchunguzi wa usalama unaondelea

Shirika la CDC pamoja na washirika wengine wa serikali kuu wanaendelea kuchunguza chanjo mpya ili kubaini ikiwa zina athari zozote kali, kwa kutumia mifumo mbalimbali ya kuchunguza usalama wa chanjo. Uchunguzi huu unaoendelea unaweza kufichua athari ambazo huenda zisingeonekana wakati wa majaribio ya kliniki.

Mtu akiwa na athari mbaya sana baada ya kuchanjwa, mtoaji huduma wake wa chanjo atatuma ripoti kwa [Mfumo wa Kuripoti Tukio Baya la Chanjo](#) (VAERS). VAERS ni mfumo wa taifa unaokusanya ripoti kutoka kwa wataalamu wa huduma za afya, watengenezaji wa chanjo, na umma kuhusu matukio mabaya yanayotokea baada ya chanjo.

Ripoti za matukio mabaya ambayo hayatarajiwi, yanaonekana kutokea mara nyingi kuliko inavyotarajiwa, au yenye mifumo isiyo ya kawaida hufuatwa na utafiti maalumu.

Uchunguzi ukionyesha kwamba chanjo haina hatari, wadhibiti wanaweza kutoa mwongozo uliosasishwa unaohusu anayepaswa kupokea au kutokupokea chanjo.

Imetengenezwa Aprili 14, 2021.

Kwa maelezo zaidi, tembelea coronavirus.ohio.gov

Kwa majibu ya maswali yako kuhusu COVID-19, pigia simu 1-833-4-ASK-ODH (1-833-427-5634).

Afya yako ya akili ni muhimu tu kama afya yako ya mwili. Ikiwa wewe au mpendwa wako anakabiliwa na wasiwasi unaohusiana na janga la virusi vya korona, msaada unapatikana saa 24 kwa siku, siku saba kwa wiki. Pigia simu COVID-19 CareLine kupitia 1-800-720-9616.